102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
JUNI 2014
Muda: Saa 2½

For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com

# MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KASSU
## Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
## KISWAHILI Karatasi ya 3

Maagizo:

- Jibu maswali manne pekee.
- Swali la kwanza ni la lazima.
- Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki-Hadithi Fupi, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
- Maswali yote yana alama sawa.

| | SEHEMU | UPEO | TUZO |
|---|---|---|---|
| A. | RIWAYA | 20 | |
| B. | DAMU NYEUSI | 20 | |
| C. | MSTAHIKI MEYA | 20 | |
| D. | USHAIRI | 20 | |
| E. | FASIHI SIMULIZI | 20 | |
| | JUMLA | 80 | |

SEHEMU A : KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA

LAZIMA

1 " Nani kadai kwamba Afrika huru haiko huru..."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Fafanua sifa nne za msemaji (alama 4)

(c) Toa mifano miwili ya mbinu za lugha katika dondoo hili (alama 2)

(d) Thibitisha kwa kutoa mifano mahususi kutoka katika riwaya hii kuwa Afrika bado haijawa huru. (alama 10)

For More Free KCSE Past Papers Visit www.freekcsepastpapers.com

SEHEMU B

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

**Jibu swali la 4 au la 5.**

2. "Uhitaji ni mojawapo wa masuala yanayoangaziwa katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine." Fafanua ukweli wa kauli hii kwa kuzingatia hadithi zozote tano. (alama 20)

3. "Hunipeleka mbali ya siku zile za asali na maziwa. Kama ungejua athari yake mwanangu wala usingeniuliza."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Tambua na ufafanue jinsi mwandishi alivyotumia fani yoyote moja kusanifu dondoo hili. (alama 4)

(c) Onyesha nafasi ya mnenaji katika hadithi hii. (alama 4)

(d) Taja na ueleze maswala yoyote manne nyeti ambayo mtunzi ameyaangazia hadithini (alama 8)

C: SEHEMU TAMTHILIA : MSTAHIKI MEYA

4. 'Hawa wanaotaka uwasikilize ni mzizi wa vizazi vya kesho! Yote yanategemea uwezo wetu.'

(i) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)

(ii) Linganua sifa za wahusika wanaohusishwa na maneno katika dondoo. (alama 8)

(iii) Fafanua maudhui yanayojitokeza katika dondoo. (alama 2)

(iv) Jadili matumizi ya methali katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 6)

**AU**

5. Jadili jinsi Timothy Arege alivyofaulu kutumia jazanda na mbinu rejeshi katika kazi yake. (alama 20)

**SEHEMU D:**

**6. USHAIRI**

Akili zangu
Zasimama ufuoni
Macho yake
Yakikagua bahari

Papa,mkali kama mauti
Anahangaisha samaki
Kwa ndaro na maringo
Daima akijigamba
Kwamba baharini
Haupo uwezo unaotisha
Wala tisho linalomweza
Wakati anaedelea kutiririka
Huku miongoni mwa samaki
Wingu zito huzuni
Lazidi uzani

Kama kwa sumaku
Samaki wanavutwa pamoja
Na nyuma ya ngao ya umoja
Wanaenda mwendo wa mbele
Wakiimba nyimbo zenye cheche

Kwa hasira zenye moto
Papa anaongeza ukali
Bali umati wa samaki
Haulegei muumano
Wala mwendo wa mbele
Kupungua kasi

Mashambulizi makali



For More Free KCSE Past papers Visit www.freekcsepastpapers.com